JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# IKISIRI ZA KONGAMANO LA KIMATAIFA LA KISWAHILI, 2024

## HAVANA, KUBA

© chalufakita

Baruapepe: chalufakita2014@gmail.com

Simu: +255 753 595 960

+255 767 959 784

**ISBN:**

Kimepigwa chapa na:

**Yaliyomo**

**Utangulizi ................................................................ vi**

**Ratiba ya Uwasilishaji wa Makala na Mijadala ................ vii**

**Makala Elekezi: "Kinachanja Mbuga, Si Chetu Pekee Tena": Kiswahili Jana, Leo na Kesho ..........................1**

*F.E.M.K. Senkoro.................................................................. 1*

**Mikakati Bora ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni ..........................................3**

*Alwiya Omar & Maryam Ismail ............................................ 3*

**Changamoto za Juhudi ya Tafsiri za Kiswahili Kutokana na Mitazamo Mbalimbali ya Historia ya Kiswahili ...............................................................................5**

*Xiaoxi Zhang.......................................................................... 5*

**Mchango wa Wanawake katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani: Mifano kutoka kwa Samia Suluhu Hassan...................................................................7**

*Ahmad Y. Sovu & Riziki Pembe Juma ..................................... 7*

**Mabadiliko ya Ukwezwa wa Wahusika Wakuu wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mjadala wa Kidayakronia kutoka Urasimi Hadi Usasaleo........................8**

*Athumani S. Ponera ............................................................... 8*

**Mchango wa Mjadala katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Burundi ....................................................................................9**

*Bamporubusa Mathieu............................................................ 9*

**Nyaraka za Kiswahili Ajami Mashariki mwa Kongo Mwishoni mwa Karne ya 19..........................................11**
*Shaibu Issa Champunga ........................................................ 11*
**Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Ulimwenguni ..................................................13**
*Mussa M. Hans ..................................................................... 13*
**Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Kuwasilisha Masuala ya Ulinzi na Usalama: Uchambuzi kutoka Vitabu Teule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto ...............14**
*Edith Lyimo........................................................................... 14*
**Fasihi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Ontolojia za Mwafrika: Uchanganuzi wa Tamthilia Teule za Said Mohamed ..............................................................................15**
*Arthur K. Muhia.................................................................... 15*
**Siku ya Kiswahili Duniani na Fursa Zake..........................16**
*Editha Adolph ....................................................................... 16*
**Ufundishaji wa Kiswahili kwa Njia Furahishi: Mbinu ya Kuongeza Uelewa na Idadi ya Wanafunzi.....................17**
*Joash J. Gambarage .............................................................. 17*
**Kunga za Fasihi ya Kiswahili Dhidi ya Taharuki ya Mporomoko wa Maadili: Uchunguzi katika Viriri vya Malezi ............................................................................18**
*Maryam Y. Mwinyi & Mnyero A. Gunda.............................. 18*
**Usawiri wa Mtoto katika Methali za Kiswahili..................19**
*Shani Omari Mchepange ....................................................... 19*
**Tafsiri ya Istilahi za Kilimo katika Zama za Utandawazi .........................................................................21**
*Onesmo Simon Nyinondi....................................................... 21*

**Ustawi wa Kiswahili Duniani: Mkabala Mpya wa Ufundishaji na Faida Zake....................................................23**
*Aldin Mutembei* ........................................................................ 23
**Matumizi ya fafanuzi za CHATGPT katika darasa la Kiswahili kwa wageni zinaweza kuongeza kiwango chao cha ujuzi wa lugha hiyo? ............................................24**
*Maria Mkunde Kanigi*.......................................................... 24
**Mchango wa Asasi za Kiswahili katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Duniani ............................................25**
*Anna Nicholaus Kyamba*.................................................... 25
**Mawasiliano ya Kielektroni na Kianalojia katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Riwaya Teule ....................................................................27**
*Yusta Violet Mganga*........................................................... 27
**Tathmini ya Kiisimu ya Kiandrosentrikia katika Kazi za Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa *Nyota ya Rehema* ya Mohamed S. Mohamed ......................................29**
*Zelda Elisifa Sam* ................................................................. 29
**Kiswahili na Fasihi: Kuanzia Lugha ya Kifasihi Hadi Lugha Kienzo ya Uhakiki...................................................31**
*Kyallo W. Wamitila*............................................................... 31
**Mchango wa Muziki wa Kiswahili kwa Utalii Afrika Mashariki..................................................................32**
*Indindi Henry* ......................................................................... 32

## Utangulizi

Kitabu hiki kina ikisiri za makala ishirini na mbili ambazo zinalengwa kuwasilishwa katika Kongamano la Kimataifa la Kiswahili litakalofanyika Havana, Kuba, kuanzia Novemba 7 hadi 10, 2024. Ikisiri zote, zikiongozwa na ile ya makala elekezi, zinaegemea katika mada kuu ya Kongamano hili ambayo ni **Ustawi wa Kiswahili Duniani: Tulikotoka, Tulipo na Tuendako**. Ikisiri hizo ni za wawasilishaji wanaotoka katika nchi mbalimbali duniani, hivyo kukamilisha dhana ya umataifa wa Kongamano hili.

Makala zinazotarajiwa kuwasilishwa zinaangazia maeneo mbalimbali ya isimu, fasihi, na utamaduni wa Mswahili. Aidha, makala hizo zinaangazia masuala mtambuko yanahusiana na lugha ya Kiswahili. Aidha, kuna makala zinazothibitisha kuwa Kiswahili kimekwishachuchuka na kuanza kubeba majukumu makubwa ya kuzisemea taaluma nyingine kama vile kilimo, mazingira, afya, ulinzi, siasa, usalama, falsafa, na TEHAMA.

Kimuundo, kitabu hiki kina masuala makubwa mawili. Nayo ni ratiba ya uwasilishaji pamoja na ikisiri. Kila ikisiri ina vipengele vifuatavyo: anwani ya makala, jina la mwasilishaji au wawasilishaji pamoja na anwani ya baruapepe. Vipengele hivi ni muhimu kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa maudhui ya makala husika kwa siku za baadaye (kwa kuwasiliana na mwasilishaji) pamoja na kuimarisha ‘usemezano wa kitaaluma’.

# Ratiba ya Uwasilishaji wa Mada na Mijadala - Kongamano la Kimataifa la Kiswahili, Havana - Kuba

**Novemba 7 – 10, 2024**

| Siku ya Pili - Ijumaa Novemba 8, 2024 | | |
|---|---|---|
| **Muda** | **Tukio** | **Wahusika** |
| **Makala Elekezi**<br>*Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Prof. Mutembei & Katibu ni Dkt. Athumani Ponera** | | |
| Saa 6:35 – 7:00 Mcha. | "Kinachanja Mbuga, Si Chetu Pekee Tena": Kiswahili Jana, Leo na Kesho | *Prof. F.E.M.K. Senkoro* |
| Saa 7:00 – 7:15 Mcha. | Mjadala wa makala elekezi | Wote |
| Saa 7:15 – 8:15 Mcha. | **Chamcha na Mapumziko** | **Wote** |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya I:**<br>*Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Dkt. Ahmad Sovu & Katibu ni Dkt. Zelda E. Sam** | | |
| Saa 8:15 – 8:35 Mcha. | Ufundishaji wa Kiswahili kwa Njia Furahishi: Mbinu ya Kuongeza Uelewa na Idadi ya Wanafunzi | *Joash J. Gambarage* |
| Saa 8:35 – 8:55 Mcha. | Ustawi wa Kiswahili Duniani: Mkabala Mpya wa Ufundishaji na Faida zake | *Aldin Mutembei* |

| | | |
|---|---|---|
| Saa 8:55 – 9:15 Alas. | Mikakati Bora ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni | *Alwiya Omar & Maryam Ismail* |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya II:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Prof. Shani Omari & Katibu ni Dkt. Maryam Mwinyi** | | |
| Saa 9:15 – 9:35 Alas. | Fasihi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Ontolojia za Mwafrika: Uchanganuzi wa Tamthilia Teule za Said Mohamed | *Arthur K. Muhia* |
| Saa 9:35 – 9:55 Alas. | *Mabadiliko ya Ukwezwa wa Wahusika Wakuu wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mjadala wa Kidayakronia kutoka Urasimi Hadi Usasaleo* | *Athumani S. Ponera* |
| Saa 9:55 – 10:15 Alas. | Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Kuwasilisha Masuala ya Ulinzi na Usalama: Uchambuzi kutoka Vitabu Teule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto | *Edith Lyimo* |
| **Siku ya Tatu - Jumamosi Novemba 9, 2024** | | |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya III:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Dkt. Joash Gambarage & Katibu ni Dkt. Yusta Mganga** | | |
| Saa 2:00 – 2:20 Asub. | Changamoto za Juhudi ya Tafsiri za Kiswahili Kutokana na Mitazamo Mbalimbali ya Historia ya Kiswahili | *Xiaoxi Zhang* |
| Saa 2:20 – 2:40 Asub. | Nyaraka za Kiswahili Ajami Mashariki mwa Kongo Mwishoni mwa Karne ya 19 | *Shaibu I. Champunga* |

| | | |
|---|---|---|
| Saa 2:40 – 3:00 Asub. | Usawiri wa Mtoto katika Methali za Kiswahili | *Shani Omari Mchepange* |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya IV:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Prof. Alwiya Omar & Katibu ni Dkt. Edith Lyimo** | | |
| Saa 3:00 – 3:20 Asub. | Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Ulimwenguni | *Mussa M. Hans* |
| Saa 3:20 – 3:40 Asub. | Mchango wa Asasi za Kiswahili katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Duniani | *Anna Nicholaus Kyamba* |
| Saa 3:40 – 4:00 Asub. | Kunga za Fasihi ya Kiswahili Dhidi ya Taharuki ya Mporomoko wa Maadili: Uchunguzi katika Viriri vya Malezi | *Maryam Y. Mwinyi & Mnyero A. Gunda* |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya V:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Dkt. Arthur Muhia & Katibu ni Dkt. Editha Adolph** | | |
| Saa 4:20 – 4:40 Asub. | Matumizi ya fafanuzi za CHATGPT katika darasa la Kiswahili kwa wageni zinaweza kuongeza kiwango chao cha ujuzi wa lugha hiyo? | *Maria Mkunde Kanigi* |
| Saa 4:40 – 5:00 Asub. | Mchango wa Mjadala katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Burundi | *Bamporubusa Mathieu* |
| Saa 5:00 – 5:20 Asub. | Tafsiri ya Istilahi za Kilimo katika Zama za Utandawazi | *Onesmo Simon Nyinondi* |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya VI:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Dkt. Mussa Hans & Katibu ni Dkt. Anna Kyamba** | | |

| | | |
|---|---|---|
| Saa 5:20 – 5:40 Mcha. | Mawasiliano ya Kielektroni na Kianalojia katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Riwaya Teule | *Yusta Violet Mganga* |
| Saa 5:40 – 6:00 Mcha. | Tathmini ya Kiisimu ya Kiandrosentrikia katika Kazi za Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa *Nyota ya Rehema* ya Mohamed S. Mohamed | *Zelda Elisifa Sam* |
| Saa 6:00 – 6:20 Adhu. | Mchango wa Wanawake katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani: Mifano kutoka kwa Samia Suluhu Hassan | *Ahmad Y. Sovu & Riziki Pembe Juma* |
| **Uwasilishaji wa Makala Awamu ya VII:** *Wasimamizi*: **Mwenyekiti ni Dkt. Maria Kanigi & Katibu ni Bw. Bamporubusa Mathieu** | | |
| Saa 6:20 – 6:40 Mcha. | Siku ya Kiswahili Duniani na Fursa Zake | *Editha Adolph* |
| Saa 6:40 – 7:00 Mcha. | Kiswahili na Fasihi: Kuanzia Lugha ya Kifasihi Hadi Lugha Kienzo ya Uhakiki | *Kyallo W. Wamitila* |
| Saa 7:00 – 7:20 Mcha. | Mchango wa Muziki wa Kiswahili kwa Utalii Afrika Mashariki | *Indindi Henry* |

# Makala Elekezi: "Kinachanja Mbuga, Si Chetu Pekee Tena": Kiswahili Jana, Leo na Kesho

Makala Elekezi kwa Ajili ya Kongamano la Kimataifa la Kiswahili

Havana - Kuba,

7-10 Novemba 2024.

*F.E.M.K. Senkoro*

femks2019@gmail.com

Ni kawaida kusikia kauli kuwa "Kiswahili kinachanja mbuga", "Kiswahili hakina wenyewe tena", na nyingine za aina hiyo. Makala hii elekezi inaonesha jinsi ambavyo, kwa kiasi kikubwa, kauli hizi zinaakisi na kukubaliana na historia na mwelekeo wa lugha ya Kiswahili na zinasawiri uhalisi wa maendeleo ya lugha hii kwa nchi mojamoja, kikanda, kwa bara zima la Afrika, na duniani kote. Makala inaangazia na kuchambua masuala ya kuzingatia ili kuendana na kasi ya kukua na kusambaa kwa lugha hii. Miongoni mwayo ni yale ya kitamaduni, nafasi ya vijana sambamba na yale ya kiteknolojia katika maendeleo ya Kiswahili, ubidhaishaji wa Kiswahili na changamoto zake, pamoja na mambo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili ndani na nje ya Afrika. Lengo ni kuchokoza mjadala kuhusu mustakabali wa lugha ya Kiswahili sambamba na kani za kihistoria, kisiasa, kijamii, kitamaduni, kiuchumi na nyinginezo kama vile uhusiano wa Kiswahili na taaluma na nyuga nyingine.

**Dhana za msingi:** *historia, mustakabali, mwelekeo*, *nafasi ya vijana*, *nyuga*, *taaluma*, *teknolojia*, *ubidhaishaji*, *ufundishaji*, *utamaduni*.

# Mikakati Bora ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni

*Alwiya Omar & Maryam Ismail*
alwiyahuseina@gmail.com & maryam.ismail@suza.ac.tz

Makala hii inahusu mikakati bora ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni, tukilenga hatua tatu muhimu zinazopendekezwa na Wiggins na McTighe (2005). Hatua ya kwanza ni kwa walimu kuweka malengo ya matokeo yanayotarajiwa, ambayo ni muhimu ili kuwapa wanafunzi mwelekeo wa nini wanapaswa kujifunza. Hatua ya pili inahusu jinsi wanafunzi watakavyofikia matokeo hayo kupitia mipango na shughuli zinazozingatia mahitaji yao. Hatua ya tatu ni kwa walimu kuchagua mbinu bora za ufundishaji, kama vile kutumia lugha lengwa kwa asilimia 90 au zaidi, kuwapa nafasi wanafunzi kushiriki zaidi darasani, kuingiza utamaduni katika ufundishaji, kuwa na mazoezi yanayoendana na mazingira ya kawaida, na kutumia teknolojia ili kuimarisha uzoefu wa lugha ndani na nje ya darasa. Hatua hizi zinaendana na mfumo wa kisasa wa kufundisha lugha ya pili kwa kutumia teknolojia (TELL) unaojumuisha vipengele kama mazingira ya kujifunzia, zana za ujifunzaji, utendaji na utoaji wa maoni, ushirikiano, na ujiendelezaji wa kitaaluma. Mfumo huu unalenga kuboresha mchakato wa kujifunza lugha kwa njia ya kipekee na ya kuvutia, ikiwasaidia wanafunzi kupata ujuzi wa lugha kwa ufanisi zaidi. Mikakati mengine bora ni kutafakari baada ya somo na kujifanyia tathmini, kutoa motisha, na kutumia ucheshi katika ufundishaji. Kujifanyia tathmini husaidia walimu kubaini maeneo ya kuboresha, huku utoaji wa motisha

kama kuwasifu na kuwapa zawadi huwahamisha wanafunzi kujifunza zaidi. Aidha, matumizi ya ucheshi darasani huongeza ushiriki na kupunguza uchovu, hivyo kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

# Changamoto za Juhudi ya Tafsiri za Kiswahili Kutokana na Mitazamo Mbalimbali ya Historia ya Kiswahili

*Xiaoxi Zhang*
xiaoxizh25@gmail.com

Kutokana na uzoefu tofauti wa hali ya ukoloni, lugha nyingi zisizo za asili ya Ulaya Magharibi zina sura mbalimbali na historia tofauti zikilinganishwa na lugha kama Kifaransa, Kiingereza, Kihispania, na Kireno. Kiswahili kinaweza kuzingatiwa kama mojawapo ya lugha za Kibantu, lugha ya asili ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki, lugha ya ujamaa, lugha ya taifa ya Tanzania na Kenya, na lugha takatifu ya ukombozi ya bara zima la Afrika kama vile watu wote duniani wenye asili ya Afrika. Kutokana na ukosefu wa hali ya masomo na usanifishaji wa lugha ya Kiswahili wakati wa ukoloni, swali la "wenyeji halali" la Kiswahili kama vile namna mwafaka wa kukitumia bado linajadiliwa sana siku hizi. Hali hii inaweza kupendekeza mielekeo tofauti ambayo lugha hii inaweza kuchukua ili kuendelea kukuza. Hali hii huzua changamoto nyingi sana kwa watafsiri wa Kiswahili, hususani watafsiri wa fasihi kutoka Kiswahili hadi lugha nyingine zisizo za Magharibi mwa Ulaya. Makala hii inafafanua mitazamo tofauti kuhusu lugha ya Kiswahili kutoka kwa watu mbalimbali wanaodai kuihusu, zamani na sasa. Aidha, inatoa maelezo mafupi ya ulinganisho wa historia ya Kiswahili na historia ya Kichina, Kiurdu, na Kireno katika makoloni ya zamani ya Ureno, ili kuonyesha changamoto hizi za kazi za watafsiri. Hoja yangu ni kuhusu umuhimu kwa wafasiri wa Kiswahili kufikia uelewa wa kina wa kihistoria wa Kiswahili. Hata hivyo, uelewa kama huo hauwezi

kupatikana bila majadiliano na ushirikiano wa wasomi, waandishi, wazungumzaji wenyeji wa lugha na kila anayefanya kazi na lugha hii kuelekea ukombozi wa kweli.

**Dhana za msingi:** Tafsiri, wafasiri na ukombozi.

# Mchango wa Wanawake katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani: Mifano kutoka kwa Samia Suluhu Hassan

*Ahmad Y. Sovu & Riziki Pembe Juma*

*sovu82@gmail.com & rizikijamal@yahoo.com*

Makala hii inalenga kujadili mchango wa wanawake katika maendeleo ya Kiswahili duniani. Mjadala unaangazia mchango wa mwanamke wa kwanza kuwa Rais katika nchi ya Tanzania, Daktari Samia Suluhu Hassan (kuanzia sasa Samia), katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Utafiti uliozaa makala hii uliangazia kipindi cha kuanzia mwezi Machi 2021 alipotawazwa kuwa rais hadi mwezi Juni 2024. Utafiti na mjadala vimeongozwa na Nadharia ya Balagha. Data zilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya usikilizaji wa hotuba na udurusu wa nyaraka mbalimbali. Matokeo yamedhihirisha kuwa Samia ana mchango ufuatao katika maendeleo ya Kiswahili: kuanzisha vituo vya Kiswahili katika ofisi za ubalozi wa Tanzania katika nchi mbalimbali, kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu, kuongeza msamiati katika Kiswahili, kuchagiza matumizi ya misemo na kaulimbiu za Kiswahili, kuhimiza ari ya uchapishaji kwa waandishi wa Kiswahili wakongwe na chipukizi, kuhimiza juhudi za nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kukuza Kiswahili, kuhimiza kuchangamkia fursa za Kiswahili, pamoja na kuendelea kutumia Kiswahili katika hafla mbalimbali za serikali. Makala inadhihirisha utashi wa kisiasa wa Samia katika ukuzaji wa Kiswahili na uzalendo wa lugha ya Kiswahili duniani.

**Dhana za msingi**: utashi wa kisiasa, maendeleo, mchango

## Mabadiliko ya Ukwezwa wa Wahusika Wakuu wa Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mjadala wa Kidayakronia kutoka Urasimi Hadi Usasaleo

*Athumani S. Ponera*

athuman.ponera@udom.ac.tz

Ukwezwa unajadiliwa katika makala hii kama mojawapo ya sifa za wahusika wa riwaya pendwa. Riwaya pendwa ya Kiswahili iliasisiwa na Muhammed Said Abdulla katika miaka ya 1960. Hivyo, ina umri wa takribani miongo saba. Hoja kuu ya makala hii ni kuthibitisha kuwa kuna mabadiliko yanayotokana na teknolojia katika kuwakweza wahusika wakuu wa riwaya pendwa ya Kiswahili yaliyotokea katika kipindi hicho. Data zimepatikana kupitia uchambuzi wa matini. Mjadala wa makala unajiegemeza katika data za wahusika watatu wanaowakilisha mihula yenye tofauti za kiwango cha teknolojia. Nao ni Bwana MSA (anayetumiwa na Muhammed S. Abdulla), Willy Gamba (anayetumiwa na Aristablus E. Musiba), na Mathew Mulumbi (anayetumiwa na Patrick C. Kafuku). Wahusika hawa wanawakilisha mihula ya urasimi, ulimbwende, na usasaleo wa riwaya pendwa ya Kiswahili mtawalia. Imedhihirika kuwa tofauti za kuwakweza wahusika wakuu hawa wa riwaya pendwa zinabainika katika vipengele vya aina, mbinu, na upeo au mawanda.

**Dhana za msingi:** Usasaleo, ukwezwa, urasimi na dayakronia

# Mchango wa Mjadala katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Burundi

*Bamporubusa Mathieu*
bamat_nven27@yahoo.fr

Mazungumzo ni mojawapo ya stadi nne za lugha. Stadi zingine za lugha ni kusikiliza, kusoma na kuandika. Umilisi wa stadi hizi unategemea mwalimu atumie muda wa kutosha na mbinu anuwai zinazomshirikisha mwanafunzi kuchangamana na wengine katika mazungumzo, michezo ya lugha, dayolojia, na mijadala inayohusu mazingira na miktadha inayoakisi hali halisi (Smith, 1995). Kwa muktadha wa vyuo vikuu nchini Burundi, wanafunzi hutumia Kirundi kwa muda mrefu wanapochangamana. Hii hutokana na kukosa umilisi mzuri wa stadi ya kuzungumza Kiswahili. Kwa hiyo, makala hii inabainisha mchango wa mjadala katika kufundisha Kiswahili cha mazungumzo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Burundi. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia mahojiano kati ya mtafiti na walimu wa Kiswahili na ushuhudiaji ambao ulifanywa katika madarasa ya wanafunzi wa mwaka wa tatu katika vyuo teule. Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Majukumu ya Robert Owen (1998). Data zilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuwasilishwa kwa asilimia na majedwali. Makala inabainisha kuwa mjadala una nafasi kubwa katika uimarishaji wa stadi ya mazungumzo kwa sababu suala hilo huhamasisha wanafunzi kuchangamana na wengine kwa mazungumzo. Makala hii inapendekeza wanafunzi kuendeleza Kiswahili cha

mazungumzo hata nje ya madarasa, hasa kwa kujiunga na mashirika yanayofundisha Kiswahili kama Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili Vyuo Vikuu nchini Burundi (CHAWAKIVIBU), na *Solution Académique pour la Promotion du Swahili Standard* (SAPROSS). Aidha, makala hii inapendekeza walimu kutumia mijadala kufundishia stadi ya kuzungumza darasani ili kuimarisha umilisi wa stadi ya mazungumzo.

**Dhana za msingi:** Stadi za mawasiliano, ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, SAPROSS, na CHAWAKIVIBU

# Nyaraka za Kiswahili Ajami Mashariki mwa Kongo Mwishoni mwa Karne ya 19

*Shaibu Issa Champunga*

shaibu.champunga12@gmail.com/shaibu.champunga@ulb.be

Makala hii inarekebisha kwa kiasi kikubwa historia ya Afrika ya Kati na kubadilisha mtazamo wa utamaduni wake, hasa kuhusu uwezo wa kusoma na kuandika na uwapo wa Kiswahili katika hati ya Kiarabu katika karne ya 19. Kuna uwapo wa nyaraka za ajami zilizoandikwa kwa lugha za Kiafrika kwa kutumia hati ya Kiarabu katika bara la Afrika. Kihistoria, utafiti kuhusu maandishi ya hati ya Kiarabu ulilenga Mashariki ya Kati, na kupuuza maeneo mengine kama Asia na Afrika ambayo pia yana utajiri wa urithi wa maandishi kama hayo. Nchi nyingi za Kasikazini mwa Afrika na zilizopo chini ya Jangwa la Sahara zina nyaraka nyingi za ajami, ikiwa ni pamoja na Hausa, Fulani, Wolof, na Maninka (Afrika ya Magharibi), na Kiswahili katika Afrika ya Mashariki (Somalia, Ethiopia, Tanzania, Kenya, Msumbiji, na Komoro), pamoja na Kiafrikana (Afrika Kusini). Historia ya Kongo haijazungumzia uwapo wa nyaraka za Kiswahili. Licha ya kuwapo kwa uzalishaji mkubwa wa maandishi ya Kiswahili kwa hati ya Kiarabu katika karne ya 19, ambayo pia yalienea hadi Burundi na baadaye Rwanda, umuhimu wa maandishi haya bado haujatambuliwa vya kutosha katika historia ya Kongo. Data za makala hii zimekusanywa maktabani kutoka katika nyaraka mbalimbali kama vile barua na mikataba ya makubaliano kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Nyaraka hizo zimehifadhiwa katika makumbusho na makavazi mbalimbali nchini Ubelgiji kama

vile *Royal Army Museum (MRA)*, *Royal Museum for Central Africa (MRAC)*, na *Tervuren*. Hivyo basi, makala hii inazitafsiri nyaraka tatu za Kiswahili ajami kutoka Maniema, Marungu na Uele. Kisha, inazitolea ufafanuzi wa kina ili kuelewa Kiswahili cha Kongo kabla ya ukoloni. Pia, inafafanua baadhi ya miktadha ya kihistoria, kiisimu na kijamii ya nyaraka hizi na athari zake katika Kiswahili.

**Dhana za msingi**: Kiswahili Ajami, nyaraka za Kiswahili, na makavazi.

# Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Ulimwenguni

*Mussa M. Hans*

hansmussa@udsm.ac.tz/ mussahans30@gmail.com

Lugha ya Kiswahili inaendelea kukua na kuenea kwa kasi katika maeneo mbalimbali ulimwenguni. Hivi sasa kumekuwa na mahitaji makubwa ya watu wanaotaka kujifunza na kutumia Kiswahili, huku wengine wakisaka vitendea kazi kama vitabu na kamusi kwa lengo la kujifunza na kufanya shughuli mbalimbali kama tafsiri na ukalimani. Maendeleo haya, mbali na mambo mengine, yanatokana na utashi wa kisiasa ambao umekuwa ukioneshwa na unaoendelea kuoneshwa na viongozi mbalimbali wa kisiasa. Nchini Tanzania, maendeleo ya Kiswahili yamekuwa yakipigiwa chapuo na viongozi waandamizi wa kisiasa na bila shaka ndiyo sababu lugha hii inaendelea kukua kwa kasi kila uchao. Kama wasemavyo wahenga, *Usione vyaelea vimeundwa*, na kwamba *ukiona Kiswahili kinakua na kuenea ujue kimekuzwa na kuenezwa na mataifa mbalimbali, ikiwamo Tanzania.* Lengo la makala hii ni kujadili mchango wa Tanzania katika ukuzaji na uenezaji wa Kiswahili ulimwenguni. Makala inaangazia mchango wa serikali za awamu ya kwanza na awamu ya sita na ya nane kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mtawalia. Data za makala hii zilipatikana kwa njia ya upitiaji wa nyaraka na usaili.

**Dhana za msingi**: Kukua na kuenea kwa Kiswahili, viongozi waandamizi, na utashi wa kisiasa

# Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Kuwasilisha Masuala ya Ulinzi na Usalama: Uchambuzi kutoka Vitabu Teule vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

*Edith Lyimo*
edithbalyimo@gmail.com

Ulinzi na usalama ni dhana ambazo zimezoeleka masikioni mwa watu, hasa pale masuala ya utulivu, amani na ustawi yanapoongelewa. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2018) inafasili ulinzi kama kazi ya kulinda, huku kulinda kukifafanuliwa kama kuweka salama au kuangalia ili kuepusha na madhara au hasara. Kadhalika, kamusi hii inafasili usalama kama hali ya kutokuwepo kwa hatari au matatizo. Kutokana na fasili hizi ni wazi kuwa kimuundo dhana hizi zinatenganishika lakini kiutendaji ni dhana zilizozoeleka kufanya kazi pamoja kwa maana kwamba zinakamilishana. Masuala haya ya ulinzi na usalama yamezoeleka katika miktadha ya kisiasa na kiutawala. Hata hivyo, masuala ya ulinzi na usalama ni muhimu kwa ustawi wa mwanadamu yeyote na katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, n.k. Makala hii inafafanua jinsi masuala ya ulinzi na usalama yanavyowasilishwa katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Vitabu hivyo ni *Mtego Kabambe* kilichotungwa na Abeid (2003) na *Wema Amwokoa Noa* kilichotungwa na Mkufya (2009). Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Tunduizi wa Vilongo kwa mujibu wa Fairclogh na Wodak (1997).

**Dhana za msingi:** Ulinzi na Usalama, fasihi ya watoto, na Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.

# Fasihi ya Kiswahili katika Ukombozi wa Ontolojia za Mwafrika: Uchanganuzi wa Tamthilia Teule za Said Mohamed

*Arthur K. Muhia*

arthurmuhiak@gmail.com

Lugha, utamaduni na ontolojia zimeingiliana kwa njia maalumu ambayo inaweza kufumbatwa kwenye tungo za kifasihi ambazo zinaakisi ontolojia na epistemolojia za lugha husika kama anavyoeleza Ngũgĩ wa Thiong'o kwenye kitabu chake cha *Decolonizing the Mind*. Maelezo yake yanaungwa mkono na mawazo ya *Sapir-Whorf Hypothesis*, Isimu-tambuzi pamoja na wananadharia wa kibaada-ukoloni kama vile Edward Said, Frantz Fanon na Homi Bhabha. Ni katika muktadha huu ambapo itikadi kuhusu suala la ukombozi wa ontolojia za Mwafrika kutoka kwenye pingu za utandawazi hasi zinajadiliwa kwa kutumia tamthilia nne za Said Mohamed: *Amezidi* (1995) *Janga la Werevu* (2011), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Uchanganuzi matini huu wa kimaktaba unaongozwa na nadharia ya Baada-ukoloni. Umuhimu wa makala hii utakuwa ni pamoja na kudhihirisha kimakusudi mitazamo ya tamthilia zilizochaguliwa kuhusu ontolojia za Mwafrika pamoja na mapendekezo ya namna za ukombozi wake dhidi ya utandawazi hasi. Vilevile, matokeo ya utafiti uliozaa makala hii yatawasaidia watunga sera zinazohusiana na suala la uhifadhi na uimarishaji wa ontolojia za Mwafrika, hasa kupitia lugha ya Kiswahili.

**Dhana za msingi**: Ukombozi wa ontolojia za Mwafrika, utandawazi hasi, na epistimolojia

## Siku ya Kiswahili Duniani na Fursa Zake

*Editha Adolph*
petereddy51@gmail.com

Siku ya Kiswahili duniani ni siku maalumu iliyotengwa na UNESCO kama siku ya kuadhimisha lugha adhimu na aushi ya Kiswahili. Maadhimisho hayo hufanyika tarehe saba mwezi wa saba kila mwaka. Siku hii imepewa jina la MASIKIDU, yaani Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. Makala hii inaangazia fursa mbalimbali zinazotokana na siku ya Kiswahili duniani. Data za utafiti zimekusanywa kwa mbinu ya ushuhudiaji, usaili na upitiaji wa nyaraka kadhaa kutoka maktabani. Makala inabainisha kwamba siku ya Kiswahili duniani ina fursa zifuatazo: kuwaleta pamoja wanataaluma na watu wengine, kupata maarifa mapya kutokana na makongamano ya kitaaluma yanayofanyika katika siku hiyo, kujenga urafiki, mauzo ya vitu mbalimbali, vikiwamo vitabu, majarida, na viongozi wa serikali kutoa matamko ya kukieneza Kiswahili. Makala hii inawahamasisha watu kuhudhuria siku hii kutokana na kuzijua fursa zinazotokana na siku hii.

**Dhana za msingi:** Fursa za Kiswahili, na MASIKIDU

**Ufundishaji wa Kiswahili kwa Njia Furahishi: Mbinu ya Kuongeza Uelewa na Idadi ya Wanafunzi**

*Joash J. Gambarage*
joash.gambarage@ubc.ca

Moja kati ya matatizo yanayoikabili tasnia ya ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni, hususani vyuoni na kwa watoto wenye urithi wa Kiswahili (*Swahili Heritage Learners*), ni kupungua kwa idadi ya watoto waliojiandikisha baada ya kuanza kusoma Kiswahili. Hii inaweza kuwa inatokana na ugumu wa sarufi ya Kiswahili. Miongoni mwa nduni tambulishi za lugha ya Kiswahili ni: (i) kuwapo kwa upatanishi mwingi wa kisarufi, (ii) idadi kubwa ya ngeli za majina, (iii) mfumo wa mkazo, na (iv) kuwapo kwa idadi kubwa ya maneno ya Kiarabu, hususani kuhesabu 10 hadi 100. Makala hii inatumia mbinu mahususi furahishi zilizobuniwa na Gambarage (2024), sambamba na fikra za Ludke (2009) na Rees (1997). Makala inabainisha kuwa idadi ya wanaojifunza Kiswahili katika madarasa ya Kiswahili nchini Kanada inaongezeka; na kwamba, wanafunzi hawalikimbii kabisa somo la Kiswahili. Mbinu hizo, kama zinavyoelezwa na Gambarage (2024) zinawashirikisha walimu na wadau wa kufunza Kiswahili duniani. Mwisho makala inajadili kwa ufupi maoni ya baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wa nchini Kanada juu ya mbinu hizo. Makala hii inatoa mchango juu ya mbinu na uboreshaji wa ufundishaji Kiswahili.

# Kunga za Fasihi ya Kiswahili Dhidi ya Taharuki ya Mporomoko wa Maadili: Uchunguzi katika Viriri vya Malezi

*Maryam Y. Mwinyi & Mnyero A. Gunda*

mayumwi@gmail.com & mwakaaje2000@gmail.com

Mporomoko wa maadili ni taharuki iliyoenea Tanzania, Afrika na ulimwenguni kwa jumla. Makala hii inajadili namna viriri vya malezi kama sehemu ya kunga za fasihi ya Kiswahili vinavyoweza kuchangia suluhisho la taharuki tajwa. Data zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayohusiana na mada tajwa, matini za kidini, sheria, taratibu na kanuni za nchi. Matokeo yanaweka bayana kwamba kunga za fasihi katika viriri vya malezi ni silaha madhubuti dhidi ya taharuki ya mporomoko wa maadili kama ilivyokuwa awali. Kwa msingi huo, jamii ina wajibu wa kuziishi kunga za fasihi ya Kiswahili ili kuvipa uhai viriri vya malezi kwa maslahi na ustawi wa vizazi vilivyopo na vinavyokuja.

# Usawiri wa Mtoto katika Methali za Kiswahili

*Shani Omari Mchepange*
shaniom@yahoo.co.uk

Methali ni kauli za hekima na uzoefu zinazozungumzia masuala mbalimbali katika jamii. Mojawapo ya masuala hayo ni kuhusu mtoto. Hivyo, katika utamaduni wa Mswahili, na kama ilivyo katika tamaduni nyingi za Kiafrika, methali ni kipera kimojawapo cha sanaajadi na fasihi kinachozungumzia masuala mbalimbali, ikiwamo kuhusu mtoto/watoto. Lengo la makala hii ni kujadili usawiri wa mtoto katika methali za Kiswahili. Kwa umahususi, makala inalenga kuchanganua usawiri wa mtoto katika methali hizo kama njia ya kuwasilisha mtazamo na utamaduni wa Waswahili kuhusiana na mtoto kupitia dhamira mbalimbali zinazofungamana nazo. Data za makala hii zilikusanywa kutoka katika vitabu vinavyohusu methali na tovuti mbalimbali. Makala inabainisha kwamba mtoto anasawiriwa kwa namna zifuatazo: kama baraka kutoka kwa Mungu, chanzo cha furaha kwa familia, kiumbe cha thamani, msaidizi, anahitaji huduma na uangalizi wa wazazi, anaweza kuwa na tabia nzuri au mbaya, ana tabia za kuzaliwa nazo na za kujifunza/kufundishwa, na ana uhusiano mkubwa sana na mama yake. Kupitia usawiri huu, dhamira mbalimbali zimebainika, ikiwamo malezi, elimu, matabaka, umoja, upendo, tabia, haki za watoto, utamaduni, dini, uchawi, urithi, na majukumu ya kijinsia na uwajibikaji. Kwa ujumla, methali za Kiswahili zilizochunguzwa zina mchango mkubwa kwa jamii katika kubainisha masuala mbalimbali ikiwamo ya kijinsia, kijamii,

kiutamaduni, kiuchumi na kifalsafa ya Kiafrika. Makala inapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu ulinganishi wa methali kutoka jamii mbalimbali kuhusiana na mada hii na nyingine ili kupata maarifa zaidi.

**Dhana za msingi:** Methali, mtoto, na usawiri.

# Tafsiri ya Istilahi za Kilimo katika Zama za Utandawazi

*Onesmo Simon Nyinondi*
onesmoni@gmail.com

Kadiri utandawazi unavyoleta watu kutoka tamaduni tofauti karibu zaidi, kuna ongezeko la hitaji la tafsiri sahihi za istilahi za kilimo ili kukuza uelewa wa kimataifa. Kuna uhusiano wa kina kati ya istilahi za kilimo na urithi wa kitamaduni katika lugha za Kiafrika, ambapo istilahi hizi zinajumuisha hekima ya kiikolojia na maarifa ya jadi ya kilimo yanayotumiwa katika muktadha wa Kiafrika na wa kiasili. Hata hivyo, tafsiri kati ya lugha za Kiafrika, hasa Kiswahili, na lugha za kimataifa huambatana na changamoto nyingi. Miongoni mwazo ni hatari ya kupoteza maana za kitamaduni na kiikolojia katika mchakato wa kutafsiri. Data za makala zilipatikana kwa njia ya upitiaji wa nyaraka na mahojiano na wataalamu wa tafsiri. Makala inafafanua uasili na mageuzi ya kihistoria ya istilahi za kilimo, kwa kuangazia misingi yake ya kijamii, kiuchumi, na kitamaduni. Makala inabainisha umuhimu wa istilahi hizi kwa kuhusisha na mienendo ya kihistoria na mabadilishano ya lugha. Pia, inaangazia hitaji la usawa kati ya usahihi wa lugha na uhifadhi wa kitamaduni katika kushughulikia utata wa tafsiri. Istilahi za kilimo zina mchango mkubwa katika kuhifadhi na kuendeleza maarifa ya jadi ambayo ni muhimu katika kilimo endelevu na uhifadhi wa mazingira. Kutokana na maudhui ya makala hii, jumuiya za wasomi na watafsiri itahamasika kuweka kipaumbele katika eneo hili kwa kuhakikisha wanaposhiriki vyakula vyetu duniani kote, mila na desturi zinazoambatana na vyakula

hivyo ziwasilishwe pia kwa ufanisi. Makala inapendekeza mbinu bora za kutafsiri zinazolenga kudumisha maana halisi za kitamaduni na kiikolojia za istilahi za kilimo. Aidha, inatoa wito wa kuanzishwa kwa mipango ya mafunzo maalumu kwa watafsiri ili waweze kushughulikia kwa ufanisi changamoto hizi na kuhakikisha usahihi na uhifadhi wa urithi wa kitamaduni.

**Dhana za msingi**: tafsiri, ikolojia, lugha za Kiafrika, zama za utandawazi, na istilahi za kilimo

# Ustawi wa Kiswahili Duniani: Mkabala Mpya wa Ufundishaji na Faida Zake

*Aldin Mutembei*

kaimutembei@gmail.com

Lugha ya Kiswahili imeendelea kukua na kuenea. Kutokea kuwa lugha ya eneo dogo na jamii chache za pwani ya mashariki mwa Afrika, Kiswahili sasa si tu kimeenea mahali pengi barani Afrika, bali kinasikika katika vyombo vingi vya habari duniani. Wakati nje ya bara la Afrika Kiswahili kimekuwa lugha ya utambulisho wa Waamerika wenye asili ya Afrika, barani Afrika, Kiswahili kimekuwa kikifikiriwa kuwa lugha ya Umajumui ambayo hatimaye itawatambulisha Waafrika katika jamii za ulimwengu. Je, ni kwa vipi lugha hii itauvaa Uafrika? Ni kwa vipi Waafrika ambao wana lugha zao mbalimbali za asili watakichukulia Kiswahili na kukikubali kuwa lugha inayowatambulisha? Maswali haya mawili ndiyo yanayojenga msingi wa makala hii. Kwa kutumia Nadharia ya Umajumuilugha wa Kiafrika (Bodomo, 2022), makala inajaribu kuonesha mkabala mpya wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii mbalimbali Afrika ambao utazifanya jamii hizo kukiona Kiswahili kuwa ni lugha ya utambulisho wao. Katika mjadala huu, pia tutaangalia faida za mbinu hii mpya.

**Dhana za msingi**: Umajumuilugha wa Kiafrika, lugha kama utambulisho, mkabala mpya wa ufundishaji wa Kiswahili

## Matumizi ya fafanuzi za CHATGPT katika darasa la Kiswahili kwa wageni zinaweza kuongeza kiwango chao cha ujuzi wa lugha hiyo?

*Maria Mkunde Kanigi*

mkanigi@mzumbe.ac.tz

Makala hii inalenga kuwasilisha matokeo ya utafiti uliofanywa katika darasa la Kiswahili kwa Wageni, muhula wa pili, kuanzia tarehe 27/3/2023 hadi 6/7/2023, Chuo Kikuu Mzumbe. Darasa hili lilikuwa na wajifunzaji wanne, ambao ni Wajerumani wenye umilisi wa lugha ya Kiingereza na ambao wana kiwango cha awali (chini) cha ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Tathimini ya ujuzi wao wa awali na wa mwisho wa lugha ya Kiswahili ulifanywa na Kipimo cha Lugha cha Kimarekani (ACTFL). Makala inafafanua kama fafanuzi zitolewazo na ChatGPT zinaongeza ujuzi wa kiwango cha lugha au la. Hivyo, ChatGPT inatumika kutoa fafanuzi za makosa ya kisintaksia ambayo ni: matumizi sahihi ya vipatanishi vya nomino (mtenda na mtendwa), vitenzi, na vivumishi. Pia, makosa ya matumizi ya njeo yalitolewa ufafanuzi na ChatGPT. Makala inabainisha kuwa matumizi ya fafanuzi za ChatGPT katika darasa la Kiswahili kwa Wageni ziliwasaidia wajifunzaji hawa kuongeza kiwango chao cha ujuzi wa lugha na kufikia kiwango cha kati (chini) cha ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Pamoja na fafanuzi nzuri za ChatGPT, mwalimu bado anahitajika kuwepo karibu na mjifunzaji ili kutoa fafanuzi kwa baadhi ya fafanuzi zisizo sahihi kulingana na somo husika.

**Dhana za msingi**: ChatGPT, upatanishi wa kisarufi, njeo, wajifunzaji, ufundishaji na ujifunzaji.

## Mchango wa Asasi za Kiswahili katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Duniani

*Anna Nicholaus Kyamba*

annanicholausk@gmail.com au anna.kyamba@out.ac.tz

Asasi za Kiswahili ni nguzo muhimu katika kukuza na kuendeleza Kiswahili Duniani. Tanzania, kama ilivyo kwa nchi nyingine, ina asasi zenye mikakati mbalimbali za kukuza na kuendeleza lugha ndani na nje ya nchi. Baadhi ya mikakati hiyo ni uundaji wa asasi mbalimbali kwa lengo la kutimiza azma hiyo. Baadhi ya asasi zilizopo Tanzania ni: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania (BAMVITA), Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), na Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (SKILUKI). Kupitia asasi hizo, Kiswahili kimeendelea kukua na kuenea duniani. Vilevile, lugha hii imeendelea kutambuliwa na kutumika na mamlaka mbalimbali za kimataifa. Kwa sasa, Kiswahili ni miongoni mwa lugha rasmi katika Umoja wa Afrika, SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Novemba 2021 shirika la UNESCO lilitangaza tarehe 7 Julai kila mwaka kuwa ni maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani. Baada ya tamko hilo, asasi mbalimbali zimeendelea kuimarisha na kuunda mikakati mbalimbali ya kuendeleza Kiswahili duniani. Kutokana na jitihada mbalimbali zinazowekwa na asasi katika kuendeleza Kiswahili, ndipo tunapata msukumo wa kuangazia zaidi mchango wa asasi za Kiswahili katika kukuza na kuendeleza Kiswahili Duniani. Katika makala hii, asasi zinazotumika ni TATAKI na BAKITA kwa upande wa Tanzania bara na BAKIZA kwa upande wa Tanzania Visiwani (Zanzibar). Tumechagua asasi

hizo kimakusudi kwa sababu ndizo zinazojishughulisha zaidi na masuala ya ufundishaji, uchapishaji na ukuzaji wa Kiswahili kuliko asasi nyingine. Pia, asasi hizi zimesaidia kuzilea asasi zingine kama vile BAMVITA.

**Mawasiliano ya Kielektroni na Kianalojia katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Riwaya Teule**

*Yusta Violet Mganga*
mgangay@yahoo.com

Taaluma ya fasihi inapitia mabadiliko ya kiwakati na kupata maendeleo katika matumizi ya mitindo ya uandishi wa kazi za fasihi. Hali hiyo imetokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Riwaya za karne ya ishirini zimeandikwa kwa kutumia mitindo inayofungamana na hali halisi ya maisha ya sasa. Miongoni mwa mitindo hiyo ni matumizi ya mawasiliano ya kielektroni na kianalojia za mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii. Katika mazingira ya kawaida, imezoeleka mawasiliano ya kielektroni na mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii si kazi za fasihi. Hivyo, kutokana matumizi hayo, ipo haja ya kuchunguza aina za mitindo hiyo, na matumizi ya lugha katika mitindo hiyo ili kubaini ufasihi wake. Lengo la makala hii ni kubainisha mitindo hiyo katika riwaya za Kiswahili. Nadharia ya Usemezano imesaidia kubainisha aina za mitindo inayotokana na mawasiliano ya kila siku katika jamii. Data za makala hii zilipatikana maktabani kupitia mbinu ya usomaji makini na kudurusu machapisho mbalimbali. Makala inabainisha mitindo ya barua, baruapepe, shajara na arafa, pamoja na matumizi tamathali za usemi kama: tashibiha, tasfida, majazi, taashira, methali, misemo na nahau. Ujitokezaji wa vipengele vya matumizi ya lugha katika mitindo hiyo unadhihirisha ufasihi uliomo katika mitindo inayotokana na mawasiliano ya kielektroni pamoja na nyaraka nyingine za mawasiliano ya

kila siku. Inatarajiwa makala hii itapanua uelewa wa aina ya mitindo ya kisasa katika kazi za fasihi miongoni mwa wanafasihi.

**Dhana za msingi:** Mawasiliano ya kielektroni, majazi, taashira, na mitindo ya uandishi wa kazi za fasihi

# Tathmini ya Kiisimu ya Kiandrosentrikia katika Kazi za Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa *Nyota ya Rehema* ya Mohamed S. Mohamed

*Zelda Elisifa Sam*

zemmangare@gmail.com

Makala hii ni tathmini ya kiisimu ya kiandrosentrikia katika kazi za fasihi ya Kiswahili kwa kutumia kitabu cha "*Nyota ya Rehema*" cha mwandishi Mohamed S. Mohamed. Androsentrikia kama mtazamo wa kitamaduni ambapo mwanamume anachukuliwa kwa ujumla kuwa kioo na kipimo cha ubinadamu na utu ina nafasi kubwa sana katika kujenga fikra potofu za utamaduni wa mfumodume. Usawa wa jinsia ni mada ambayo imeshika kasi hasa wakati huu wa dunia ya utanzawazi. Tanzania na kote duniani kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa tamaduni za jamii mbalimbali. Kuna baadhi ya jamii ambazo zina mwelekeo wa kuuenzi mfumo dume na zile ambazo ni kinyume chake. Mila na desturi katika jamii vinaonyesha wazi mtanzamo wa jamii moja hadi nyingine kuhusu usawa wa kijinsia kulingana na matumizi ya lugha katika jamii husika. Waandishi wengi wa vitabu, wakiwamo wa lugha ya Kiswahili, wamechukua jukumu kubwa la kuweka tamaduni mbalimbali katika vitabu na hasa wanapokuwa wanaangazia maswala kama siasa, uchumi, elimu, biashara. Nadharia ya Lynch (2023), mbinu ya usomaji makini na uchambuzi wa kimaelezo vilitumika kuibua mtazamo wa kijinsia katika kazi ya fasihi inayoangazia tamaduni zetu. Makala inadhihirisha usawiri wa kiisimu katika aina ya tungo, semantikia ya maneno pamoja na vitendo wanavyofanya wahusika, kuashiria mkabala wa kiandrosentikia. Pia, inabainisha jinsi lugha ya kifasihi ya

Kiswahili inavyotumika kujenga, kuimarisha na kubomoa juhudi za usawa wa jinsia.

**Dhana za msingi**: androsentrikia, utamaduni, jinsia

# Kiswahili na Fasihi: Kuanzia Lugha ya Kifasihi Hadi Lugha Kienzo ya Uhakiki

*Kyallo W. Wamitila*
wamitila@gmail.com

Uhusiano uliopo baina ya lugha yoyote ile na fasihi yake ni muhimu na huwa msingi muhimu wa mijadala yoyote inayohusiana na maana ya kifasihi na fasili zake katika matini na kazi za kifasihi. Waandishi, wahakiki, wanaujumi na wasomi wa fasihi wanakubaliana kuwa lugha ya fasihi hufumbata sehemu muhimu ya tajriba ya mwanadamu. Baadhi ya nadharia za kihakiki huelekeza na husisitiza umuhimu wa uchunguzi wa lugha ili kuweza kuielewa maana ya kifasihi. Kwa upande mwingine, suala la lugha ya fasihi na lugha-kienzo ya uhakiki wa matini ya fasihi huchochea mijadala na maswali ya kila aina. Je, ipo lugha ya kifasihi ambayo inahusishwa tu na fani hiyo tu? Je, yapo matumizi ya lugha katika matini na kazi za kifasihi ambayo yanahusishwa na jinsi fulani mahsusi? Je, lugha huwasilisha maana kwa uwazi tu au pia kwa kimya chake? Je, suala la kufumbata tajriba ya mwanadamu katika fasihi linahusishwa na misingi yoyote ile? Je, tunawezaje kuhusisha suala la lugha na la nadharia za kihakiki? Je, lugha-kienzo ya uhakiki katika taaluma ya fasihi imepitia hatua zipi na inasahilisha au kutatiza uelezaji na uelewekaji wa maana na fasihi Dhamira ya makala hii ni kuangalia maswali na mijadala hiyo katika muktadha wa lugha ya Kiswahili na ukuaji wa taaluma ya uhakiki. Lengo la kimsingi si kutoa ufumbuzi bali kuchochea mijadala muhimu katika fani ya uchanganuzi wa matini na kazi za kifasihi.

# Mchango wa Muziki wa Kiswahili kwa Utalii Afrika Mashariki

*Indindi Henry*

henryindindi@gmail.com

Utalii huchangia takribani asilimia 10 ya uchumi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Huu ni mchango mkubwa, hasa ikizingatiwa nafasi za ajira zinazotolewa na sekta hiyo. Miongoni mwa vivutio vya watalii katika kanda hii ni fukwe za bahari, mashamba ya mazao mbalimbali, mbuga za wanyama, mapisi na tamaduni za jamii za kanda hii. Wasanii wa muziki wa Kiswahili kutoka ukanda huu wamechangia ufanisi wa utalii huu katika tungo zao kwa kutambua na kusifia vito mbalimbali vinavyoweza kuwa vivutio vya watalii katika kanda hii. Katika makala hii, tunatambua baadhi ya muziki wa Kiswahili ambao umechangia juhudi za uchumi wa kitalii na kupambanua jinsi ujumbe huo utakavyokuza utalii. Utafiti ulifanywa kwa kusoma kuhusu maeneo yanayotembelewa kwa kiwango kikubwa na watalii na kusikiliza muziki wa Kiswahili uliotaja baadhi ya mambo kuhusu sehemu hizo. Tulipakua na kusikiliza miziki mbalimbali ya Kiswahili kutoka kwa wasanii wakongwe na wa sasa ili kubaini ujumbe wa kitalii au unaotaja sehemu za kitalii kwa njia ya kuchangia shughuli za kitalii katika ukanda huu.

**Dhana za msingi:** Utalii, muziki wa Kiswahili, na wasanii


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
wizara_sanaatz
sanaatv